

Please check the examination details below before entering your candidate information

Candidate surname

Other names

Centre Number

Candidate Number

--	--	--	--	--

--	--	--	--	--

Pearson Edexcel International GCSE (9–1)

Friday 31 May 2024

Morning (Time: 2 hours 15 minutes)

Paper
reference

4SW1/01

Swahili

PAPER 1: Reading, Writing and Translation

You do not need any other materials.

Total Marks

Instructions

- Use **black** ink or ball-point pen.
- **Fill in the boxes** at the top of this page with your name, centre number and candidate number.
- There are **three** sections you must answer:
 - Section A Questions 1–4
 - Section B Questions 5 and **either** Question 6(a) **or** 6(b) **or** 6(c)
 - Section C Question 7.
- Answer the questions in the spaces provided
 - *there may be more space than you need.*
- You must **not** use a dictionary.

Information

- The total mark for this paper is 80.
- The marks for **each** question are shown in brackets
 - *use this as a guide as to how much time to spend on each question.*

Advice

- Read each question carefully before you start to answer it.
- Check your answers if you have time at the end.

Turn over ►

P75565A

©2024 Pearson Education Ltd.
E:1/1/1/1/1




Pearson

SECTION A: READING

Answer ALL questions.

Write your answers in the spaces provided.

Multiple-choice questions must be answered with a cross in a box ☒. If you change your mind about an answer, put a line through the box ☒ and then mark your new answer with a cross ☒. Open-response questions do not have to be written in full sentences and you may respond using single words or phrases.

- 1 Malizia sentensi zifuatazo kwa **Kiswahili** na tumia taarifa katika maelezo. Weka alama sahihi kwenye kila kisanduku.

Ajali

Ninaitwa Mahir. Wikendi iliyopita, mimi na rafiki yangu Amin tulikuwa tukiendesha baisikeli zetu mtaani kwetu. Mara paka mweusi akavuka barabara na nilipojaribu kumkwepa aliruka na kunifanya nishtuke kwa woga na niachilie usukani wa baisikeli yangu. Ghafila nikadondoka chini na baisikeli yangu ikagonga ukuta. Hapo tena nikajikuta nimeumia na nikalazimika kukaa sakafuni. Tatizo ni kwamba yule paka alitoka kwenye kichaka kwa hivyo sikumwona hadi alipokuwa mbele yangu.

Lakini kitu kilichoniudhi hasa ni vile Amin alivyokuwa akicheka. Alishika tumbo huku akinicheka kwa kelele. Mara watoto wengine wakaja kunizunguka. Nilitamani kusimama lakini magoti yangu yaliuma sana. Baisikeli yangu ilionekana kuwa sawa.

- | | | | |
|-------------------|---------------------|------------------|--------------------|
| A woga | B tumbo | C kuchoka | D baisikeli |
| E kichaka | F barabarani | G kucheka | H ukutani |
| I hasira | J maumivu | K wikendi | L viungo |
| M pikipiki | | | |

Example:	Ajali ilitokea siku ya ...	K
1(a)	Usafiri aliotumia ...	
1(b)	Kulikuwa na mnyama ...	
1(c)	Alidondoka kutokana na hisia ya ...	
1(d)	Alikaa sakafuni kutokana na ...	
1(e)	Kicheko cha Amin kilimfanya Mahir ahisi ...	
1(f)	Mahir alihisi maumivu kwenye ...	

(Total for Question 1 = 6 marks)



DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

BLANK PAGE



- 2 Weka alama katika visanduku **10** vilivyo sahihi. Sentensi nyingine au watu wengine wanaweza kuwa na alama zaidi ya moja au bila alama yoyote.

Michezo nje ya shule

Asha



Mimi huogelea kwenye bwawa karibu na nyumbani kila asubuhi kabla ya kuenda shuleni. Ninahisi zoezi limenisaidia kujiamini hasa kwani ninakutana na watu wapya. Ninapenda mno kuwa kwenye maji. Baadaye nitajaribu kuogelea mtoni na baharini ingawa ninaogopa kasi za mawimbi.

Sabrina



Nimejisajili katika kilabu cha kuchora ili niweze kutuliza akili yangu. Mimi huenda mara moja kwa wiki siku za Jumamosi. Nina shauku kubwa ya kuenda ingawa hadi leo nimekutana na watu wachache sana kwani huhisi haya kusemesha watu nisiowajua.

Hirsi



Siwezi kuishi bila mpira wa miguu, hivyo huchoza kila Jumapili. Kwa vile mimi ni mchezaji mzuri sana nahodha wa timu za mpira wa miguu hunigombania. Kila mmoja hutaka nicheze katika timu yake. Mpira unanilazimisha kufuata kanuni zilizopangwa na kocha. Nimejifunza kuwa makini ninapolazimika na hii imenisaidia kufuzu katika masomo.



		Asha	Sabrina	Hirsi
Mfano:	Yupo kwenye timu	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
A	Shughuli inamsaidia kutulia	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
B	Amechagua shughuli yenye mazoezi	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
C	Hufanya shughuli mara moja kwa wiki	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
D	Shughuli inaweza kuwa hatari	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
E	Anafaulu zaidi darasani	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
F	Amekutana na watu wapya	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
G	Hufanya shughuli asubuhi	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>

(Total for Question 2 = 10 marks)



- 3 Soma makala kuhusu safari jangwani. Malizia taarifa kwa kutumia namba au maneno kwa **Kiswahili**.

Safari jangwani

Nina bahati ya kuwa na wazazi ambao wanapenda kusafiri. Tatizo lililopo ni sehemu wanazopenda kuenda: jangwani. Huko kuna ulimwengu ambao una joto kupita kiasi wakati wa mchana na baridi iliyozidi kikomo usiku. Sijawahi kumsikia mtu yeyote anayependa kutembelea jangwa. Binafsi nisingechagua kupanda ngamia na kutembea nao kwenye mchanga wa jangwa.

Ninadhani ningefurahi mno kuota jua kwenye ufukwe wa bahari ya Hindi ambapo maji yana rangi za buluu na kijani na pia kusafiri baharini kwa jahazi kubwa huku muziki wa taarab ukipigwa.

Amini usiamini, mwezi Agosti mwaka huu, wazazi wangu waliniarifu kwamba tutaenda kutembelea jangwa la Sahara! Niliposikia habari hii nilikuwa nimeketi kwenye sofa letu kubwa ambapo nilistarehe huku nikinywa soda baridi na papo hapo nilitamani kulia.

Nikauliza 'hatutaenda ufukweni bali tutaona vumbi la jangwa?' Wazazi wangu walisema 'usifanye ubishi, utafurahia ukifika huko'.

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA



Mfano: Mapenzi ya wazazi: **Safari**

(a) Hali ya hewa jangwani: na
..... (2)

(b) Shughuli **moja** ya kufanya jangwani: (1)

(c) Shughuli ambazo yeye angependa kufanya: na
..... (2)

(d) Elezea mawazo **mawili** yanayohusu wazazi mwaka huu:
..... na (2)

(e) Alichokuwa akifanya alipopata taarifa ya likizo:
na (2)

(f) Hisia yake kuhusu safari: (1)

(g) Hoja za mwisho za wazazi kuhusu safari: na
..... (2)

(Total for Question 3 = 12 marks)



- 4 Soma habari ifuatayo kutoka kitabu kiitwacho **Peponi**, kilichoandikwa na Abdulrazak Gurnah.

Yusuf

Wakati wa magharibi, Yusuf alikaa kwenye baraza pamoja na Hamid na wageni waliokuja na alihitajika kuwaletea wageni maji na sharubati kwenye bilauri kubwa.

Usiku inapokuwa baridi sana milimani au inaponyesha mvua, aliwaletea mablanketi. Walikaa juu ya mikeka, wakiizunguka taa ya kandili iliyokuwa sakafuni. Yusuf ambaye alikaa kando kutokana na umri wake mdogo, alisikiliza mikasa ya maeneo kadha wa kadha yaliyokuwa ya ajabu.

Kuna wakati walishusha sauti zao na kukaribiana, na kumfukuza Yusuf kila alipowakaribia. Hapo tena aliona macho ya wasikilizaji yakipanuka kwa msisimuko na mshangao, na mwishoni nyuso zao zilijaa vicheko walivyoangua.

Usiku mmoja alikuja mtu kutoka Mombasa akawaeleza kuhusu ami yake aliyerudi kutoka nchi ya Urusi baada ya miaka kumi na tano. Aliwastaajabisha kwa kusema kwamba kuna mji wa Petersburg ambapo katika majira ya joto jua liling'aa hadi usiku wa manane na majira ya baridi ilikuwa giza muda wote.

Ilipokuwa baridi, maji yaliganda na kuwa theluji iliyotanda juu ya mito na maziwa. Tena ilikuwa nzito hata mtu angeweza kuendesha gari la mkokoteni lililosheheni. Pia watu walitoboa mashimo kwenye theluji ili kuvua samaki.

Jibu maswali kwa **Kiswahili** na tumia taarifa katika maelezo. Si lazima kuandika sentensi kamili.

- (a) Wageni walikunywa nini?

(1)

- (b) Kuna vifaa gani pale wanapokaa?

Taja vifaa **viwili**.

(2)



(c) Kwa nini Yusuf alitengwa?

(1)

(d) Wageni walifanya nini baada ya kusikia masimulizi?

Taja maelezo **mawili**.

(2)

(e) Ukweli gani kuhusu Petersburg uliwashangaza wasikilizaji?

Taja maelezo **mawili**.

(2)

(f) Tunaambiwa nini kuhusu mito na maziwa?

Taja maelezo **mawili**.

(2)

(Total for Question 4 = 10 marks)

TOTAL FOR SECTION A = 38 MARKS



SECTION B: WRITING

Answer Questions 5 and either Question 6(a) or 6(b) or 6(c).

Write your answers in the spaces provided.

5

Zawadi

Zawadi uliyopewa

Mawazo kuhusu zawadi

Nyakati za kutoa zawadi

Zawadi pendwa za
baadaye

Andika takriban maneno 70 kwa **Kiswahili** kuhusu zawadi. Ni lazima kutumia maneno yote yaliyotajwa hapo juu.

(12)

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA



DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

Handwriting practice area with 25 horizontal dotted lines.

(Total for Question 5 = 12 marks)



P 7 5 5 6 5 A 0 1 1 1 6

- 6 Chagua **moja** kati ya maswali matatu yafuatayo na andika takriban maneno 130 kwa **Kiswahili**.

Chaguo 1



- (a) Andika hotuba kuhusu masuala ya mazingira. Ni lazima uandike kuhusu:

- Umuhimu wa kuelewa suala la mazingira
- Mambo uliyofanya nyumbani na shuleni kusaidia mazingira
- Baadaye mazingira yatakuwaje.

(20)

Chaguo 2

- (b)

Mpendwa Hannah

Sasa nimeamua kuenda kusoma chuo kikuu na kutosafiri ili kuona dunia baada ya kumaliza masomo yangu ya upili.

Je, wewe una mpango gani?

Rafikiyo,

Aaliyah

Jibu kwa kutumia barua pepe. Ni lazima uandike kuhusu:

- Mawazo yako kuhusu kusoma chuo kikuu
- Utafanya nini baada ya masomo ya upili
- Umezungumza na nani hivi karibuni kuhusu mipango yako.

(20)

Chaguo 3

- (c) Kwenye ukurasa wako wa blogu andika kuhusu ajira. Ni lazima uandike kuhusu:

- Ajira inayokuvutia zaidi
- Kazi walizofanya wazee wako walipokuwa vijana
- Jinsi ajira itakavyobadilika miaka ijayo.

(20)



DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

(Total for Question 6 = 20 marks)

TOTAL FOR SECTION B = 32 MARKS



DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

BLANK PAGE

Source Information

Question 2

© Vladimir Vladimirov/Getty Images

© SDI Productions/Getty Images

© Tassii/Getty Images

Question 6

© ilyaliren/Getty Images

